***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 30.
2. Katika karatasi ya majibu, hakikisha umeandika:-
   *(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako* *iii). Nambari ya KNEC*

***Muda:Saa 1 Dak 40***

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu swali la 1 hadi la 5.**

***(Dalton na Musila wametoka shuleni jioni wakielekea nyumbani. Njiani, wanajadiliana kuhusu masomo ya shuleni mwao.)***



**Dalton** : Siku hizi nimeanza kukichangamkia Kiswahili zaidi ya kitambo. Kinanifurahisha sana ***(Anapunguza kasi ya mwendo)***

**Musila** : Haunishindi, kwanza tunapofunzwa kuhusu mavazi, mimi hufurahi na kuelewa.

**Dalton** : Nikumbushe mwalimu alisema nini kuhusu mavazi jana? ***(Anajikuna kichwa)***

**Musila** : Hahaha! Dalton, unasahau haraka sana. Mwalimu alisema kuwa kuna mavazi ya kike na kiume.

**Dalton** : ***(Huku akitabasamu)*** Naam, nakumbuka japo nakusihi unikumbushe vyema.

**Musila** : Kunayo mavazi ya kike na kiume. Mavazi ya kike ni kama vile gagro, shimizi.....

**Dalton** : Nashukuru sana kwa kunikumbusha.

**1.** Mazungumzo haya yanafanyika wapi?
A. Shuleni B. Njiani
C. Nyumbani D. Sokoni

**2.** Kati ya mavazi haya, ni vazi lipi huvaliwa na wanawake pekee?
A. Sidiria B. Tai
C. Kanzu D. Soksi

**3.** Kulingana na mazungumzo haya, ni wazi kuwa
A. wanafunzi hawa hawajivunii Kiswahli
B. wanafunzi hawa wanasoma shule tofauti
C. wanafunzi hawa hawapendi masomo
D. wanafunzi hawa wanadhamini Kiswahili

**4.** Mazungumzo haya yanafanyika wakati gani?
A. Mchana
B. Adhuhuri
C. Jioni
D. Usiku

**5.** Mazungumzo haya ni baina ya watu wangapi?
A. Wanne
B. Wawili
C. Sita
D. Hatujaambiwa

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 6 hadi la 10.**

Moto husemekana kuwa ni mtumishi mwema lakini mkali. Binadamu hutumia moto kwa njia nyingi. Hizi ni pamoja na kupika chakula, kuchemsha maji ili kuua viini na kujiondolea baridi. Viwandani, moto hutumika kuyeyusha madini na kuunganisha vyuma. Hakika, moto ukitumika kwa njia ifaayo, huleta manufaa chungu nzima.

Kwa upande mwingine, matumizi ya moto pasipo uangalifu huweza kuzua masikitiko tele. Wapo adinasi waliowahi kuachwa na majereha mabaya au kuteketea hadi kufa kutokana na hasira za moto. Kila uchao, tunasikia visa vya kuteketea kwa nyumba, magari misitu, shule, kumbi za sherehe, maduka na maeneo mengi. Jambo kama hilo likitokea, husababisha hasara isiyokadirika.

Ni vyema kutumia moto kwa uangalifu. Tukumbuke kuwa hata cheche ya moto huchoma msitu. Watoto hawafai kuchezea viberiti au vijinga vya moto. Hata pale wanapowasha majiko ya gesi, mafuta makaa au umeme pawe na mtu mzima ambaye atasaidia kukabiliana na dharura yoyote iwapo itatokea.

**6.** Moto ni mtumishi mwema lakini mkali kwa sababu
- A. hutukinga dhidi ya baridi, hufanikisha mapishi
- B. huchoma maduka, hufanya watu kupoteza maisha
- C. hutumiwa katika ufundi, husababisha hasara ya mali
- D. huteketeza magari, husababisha majeraha

**7.** Hasara ya moto hutokea hasa ikiwa
- A. umezuka ghafla
- B. umetumiwa na watoto
- C. umewashwa pasipofaa
- D. umetumiwa bila uwajibikaji

**8.** Neno **adinasi** kama ilivyotumika ni kisawe cha
- A. watu
- B. moto
- C. hasara
- D. wahalifu

**9.** Watoto wanashauriwa wafanye nini?
- A. Wasitumie moto
- B. Waogope moto
- C. Wawe na watu wazima karibu wakitumia moto
- D. Wasiogope kutumia moto kwani hauna madhara

**10.** Ni kichwa kipi kifaacho **zaidi** kwa kifungu hiki?
- A. Faida za moto
- B. Madhara ya moto
- C. Faida na hasara ya moto
- D. Jinsi ya kutumia moto

**<u>Soma makala haya kisha ujibu swali la 11 hadi la 15.</u>**

Furaha siku zote hupatikana kwa mtu anayeitafuta, jambo lililo kinyume chake huzuni. Huzuni humpata mtu ambaye ameamua kuhuzunika. Mathalani, ukiwa hutaki kukasirika ama kuhuzunika, unaweza kuamua kumpuuza mtu ambaye amedhamiria kukuudhi. Na endapo umeamua kughadhabika na kuhuzunika na tabia ndogo, yatosha kukuchemsha nyongo. Kufurahi au kuhuzunika ni tabia za mtu binafsi. Aidha ni chaguo la mtu mwenyewe. Hiyo ndiyo sababu niliwafunza wanafunzi wangu wakati mmoja kuwa mtu akikuuliza, "Mbona una furaha leo" Mpe jibu kwamba, "Nina furaha kwa sababu sina huzuni"

**11.** Taarifa inatuambia kwamba ukiitafuta furaha
- A. huipati
- B. huwezi kuipata
- C. ni kazi bure
- D. utaipata

**12.** Ikiwa hutaki kukasirika, unaweza kuamua
- A. kumwudhi mtu
- B. kufurahi
- C. kughadhabika
- D. kuhuzunika

**13.** **"Mtu binafsi"** ni
- A. mtu mwenyewe
- B. ofisi ya mtu
- C. ufuasi wa mtu
- D. nafasi ya mtu

**14.** **"Kuchemka nyongo"** ni
- A. kucheka
- B. kupata jasho
- C. kukasirika
- D. kupika chakula

**15.** Taarifa hii inatushauri nini?
- A. Tukasirike daima
- B. Tuhuzunike daima
- C. Tufurahi na kukasirika
- D. Tuchague hali iliyo na manufaa



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 16 hadi la 20, kwa kutumia jibu bora zaidi.**

Kucheza ni kitu kizuri __16__ kucheza kupita kiasi nakufai. Mwanafunzi mzuri ni ___17____ anayejua wakati wake ___18____. Anajua wakati wa kucheza na wakati wa kusoma. ___19____ tunajua kuwa mchezo husaidia ____20____ afya zetu na kuchangamsha akili ili ziweze kufanya kazi nzuri.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **16.** | A. ila | B. wala | C. na | D. ama |
| **17.** | A. wale | B. kule | C. pale | D. yule |
| **18.** | A. mzuri | B. vizuri | C. kuzuri | D. pazuri |
| **19.** | A. Wote | B. Zote | C. Nyote | D. Sote |
| **20.** | A. kuinua | B. kuimarisha | C. kutumbuiza | D. kuangamiza |

**Kuanzia swali la 21 hadi la 30, chagua jibu lifaalo zaidi kulingana na maagizo uliyopewa.**

**21. Upi ni ukubwa wa sentensi hii?**
Mguu wa mtoto mchanga ni mdogo sana
A. Kiguu cha kitoto kichanga ni kidogo sana
B. Jiguu la jitoto changa ni ndogo sana
C. Guu la toto changa ni dogo sana
D. Jiguu la jitoto jichanga ni kidogo sana

**22.** Nomino **"kiti"** iko katika ngeli gani?
A. KI-VI
B. A-WA
C. I-ZI
D. LI-YA


**23.** Ni sentensi gani iko katika wakati uliopo?
A. Mama hajala
B. Mama hali
C. Mama hakula
D. Mama hatakula

**24.** Kauli **"kaka ni kinyonga"** ina maana kuwa
A. ana maneno mengi
B. hana siri
C. anapenda kutembea
D. ni kigeugeu

**25. Tegua kitendawili kifuatacho**
Popote niendapo yeye hunifuata.
A. Njaa
B. Jua
C. Kivuli
D. Upepo

**26.** Kipindi cha miaka kumi ni
A. mwongo
B. karne
C. milenia
D. kikwi

**27.** Maumbo haya ni



A. moyo, pembe tatu pacha
B. pia, pembe tatu pacha
C. kopa, pembe tatu
D. mstatili, pembe tatu

**28.** Neno linaloweza kutumika kuomba msamaha kwa kosa ulilofanya ni?
A. Tafadhali
B. Sitarudia
C. Hongera
D. Niwie radhi

**29.** Masalkheri ni salamu za
A. asubuhi
B. adhuhuri
C. jioni
D. mchana

**30.** **Sharafa, kope, malaika, nyusi** kwa jina moja ni
A. nywele
B. viungo
C. manyoya
D. mapambo



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

## Sehemu ya B: INSHA

| JINA LAKO | |
|---|---|

**Ufuatao ni mwanzo wa insha. Iendeleze kwa maneno yako mwenyewe huku ukiifanya iwe ya kusisimua zaidi;**

Zilikuwa zimebaki siku chache ili tufunge shule. Siku hii, nilikuwa nimeingoja kwa hamu na ghamu kwa sababu ..........................................................................................................



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com